# Haki na Majukumu ya Mgonjwa

Children's Health℠ inamhakikishia kila mgonjwahaki ya kupokea huduma inayotolewa kwa njia ya uzingatifu, heshima, hadhi na kuridhisha. Ukiwa mzazi, mlezi au mwakilishi aliyeidhinishwa wa mgonjwa kwenye Children's Health, una haki ya kupokea taarifa kuhusu haki zako na sera za hospitali zinazohusiana na haki hizo.

## Mkiwa wazazi, mna haki ya:

- **Kushiriki** kikamilifu katika maamuzi kuhusu huduma ya matibabu ya mtoto wako.
- **Kutarajia** jibu linalofaa kwa ombi lolote linalofaa kwa huduma ndani ya uwezo wa Children's Health, dhamira yake illiyobainiswa na sheria.
- **Kujua** majina ya madaktari, wauguzi na watoa huduma wengine wa afya wanaomhudumia mtoto wako.
- **Kudumisha** matibabu ya faragha na ya siri ya mawasiliano na rekodi zote kuhusu huduma ya mtoto wako ndani ya mipaka ya sheria.
- **Kuambiwa** na daktari, kwa maneno au lugha unayoelewa kuhusu ugonjwa, tiba na matarajio ya kupona.
- **Kupokea** taarifa nyingi unavyohitaji ili kuagiza kutoa au kukataa kibali kwa tiba yoyote inayopendekezwa.
- **Kufanya** maamuzi, kwa ushauriano na daktari wa mtoto wetu, kuhusu huduma ya afya ya mtoto wako. Hii inajumuisha haki ya kukubali au kukataa huduma ya matibabu kwa mtoto wako inavyokubaliwa na sheria na kuambiwa kuhusu madhara ya matibabu ya ukataaji kama huo.
- **Kukamilisha** agizo la mapema (kwa mfano, "wasia ulipo") kwa mtoto wako inavyoruhusiwa kisheria na kutarajia watoa huduma wa afya wa mtoto wako kutii agizo lolote kama hilo.
- **Kutarajia** udhibiti bora wa maumivu ya mtoto wako.
- **Kushiriki** katika masuala ya maadili kuhusu huduma ya mtoto wako.
- **Kutumia** simu kupiga na kupokea simu na kujua kuwa vikwazo vyovyoe vya sababu za matibabu vitajadiliwa nawe.
- **Kufikia** rekodi za matibabu ya mtoto wak ndani ya muda unaofaa.
- **Kuwa na** mwanafamilia au mwakilishi unayetaka na daktari wa mtoto wako kufahamishwa kuhusu kulazwa kwa mtoto wako.
- **Kumhudumia** mtoto wako kwa starehe na hadhi ikiwa anaaga dunia. Hii ni pamoja na kudhibiti maumivu ya mtoto wako, kutibu dalili zinazokubali matibabu na kutambua mahitaji ya utamaduni, kiroho na huzuni yako, mtoto wako na familia yako.

- **Kupokea** huduma ambayo haina unyanyasaji wala dhulama kutoka kwa yeyote.
- **Kumfanya** mtoto wako kutokuwa na vikwazo vya kimwili au matibabu ambavyo si muhimu kimatibabu.
- **Kumfanya** mtoto wako kutokuwa na vikwazo au kutengwa kwa ajili ya udhibiti wa tabia isipokuwa iwe hali ya dharura.
- **Kupokea** huduma katika mazingira salama.
- **Kutendewa** kwa uzingatifu na heshima bila kuangalia mbari, rangi, asili ya taifa, jinsia, dini, utambulisho wa jinsia, mvuto wa jinsia, ulemavu, msingi wa utamaduni, uchumi au elimu.
- **Kukataa** kushiriki katika mradi wowote wa utafiti unaoathiri huduma na tiba ya mtoto wako.
- **Kuwa** huru kuwasilisha malalamishi na kupokea maoni.
- **Kupata** usaidizi kuwasiliana na huduma za ulinzi inapohitajika

## Mkiwa wazazi, mna haki ya:

- **Kuambiwa** chochote kinachohitajika kuelewa sababu ya kuwa hapa.
- **Kuambiwa** haswa kitakachotendeka na jinsi hali itakavyokuwa haswa.
- **Kupewa** majibu ya kueleweka ya maswali yoyote au wasiwasi ulio nao kuhusu tiba.
- **Kumwambia** kila mtu unachofikiria na kuhusu tiba yako na ulichopangiwa.
- **Kujua** kuwa ukiwa na maumivu watu wanaokuhudumia watakusikiliza na kukusaidia kuhisi vyema.
- **Kuwa na** nyakati na sehemu za kucheza na kujifunza.
- **Kuambiwa** na watu wanaohitaji kuugusa mwili wako haswa kile watakachokifanya na kuwa watafanya hivyo taratibu na kwa njia ya faragha.
- **Kuwa** na familia yako kadri ya muda unaotaka, inapowezekana.
- **Kupata** usaidizi kujua jinsi ya kujihudumia unapoenda nyumbani.
- **Kukasirika** kulia, au kusema usichokipenda kuhusu kinachokutendekea.
- **Kupokea** wageni wanaoteuliwa na mzazi. Mzazi anaweza kuondoa au kukataa uteuzi huu wakati wowote.

## Mkiwa wagonjwa na wazazi, mna jukumu la:

- **Kuuliza** maswali wakati huelewi kile ambacho umeambiwa kuhusu huduma.
- **Kutoa** taarifa sahihi na kamili kuhusu masuala yanayohusiana na afya ya mzazi.
- **Kufuata** mpango wa tiba uliokubaliwa na wewe na timu yako ya huduma ya afya.
- **Kuzungumza** na daktari wako kuhusu unachotarajia kuhusu maumivu na udhibiti wa maumivu.

- **Wajali** wagonjwa wengine.
- **Fuata** sheria na kanuni za hospitali.
- **Ripoti** hatari zinazodhaniwa kwa uangalifu na mabadiliko yasiyotarajiwa katika hali ya mgonjwa.

## Tunakuhimiza uzungumze na:

- Muuguzi au daktari wa mtoto.
- Meneja au mkurugenzi wa uuguzi.
- Mwakilishi wa uhusiano kwa wageni kwa Simu ya Usaidizi 214-456-2273.
- Msimamizi wa uuguzi (saa za jioni au wikendi, piga simu 214-456-7000).

Ikiwa wewe au familia yako inahisi haki zako ukiwa mgonjwa hazikutimizwa, una haki ya kuwasilisha malalamishi na kupokea jibu la maandishi kutoka Grievance Resolutions Committee of Children's Health au wasilisha malalamishi kwa moja ya mashirika yaliyo hapa chini.

Ukihisi kuwa matatizo yako hayatatuliwi wala kushughulikiwa na Children's Health, unaweza kuwasiliana na:

**The Joint Commission Office of Quality and Patient Safety**
One Renaissance Boulevard
Oakbrook Terrace, Illinois 60181
**patientsafetyreport@jointcommission.org**

**Health Facility Compliance Group**
(MC 1979)
Texas Department of State Health Services
P.O. Box 149347
Austin, Texas 78714
hfc.complaints@dshs.state.tx.us
1-888-973-0022 Simu ya Dharura ya Malalamishi
1-512-834-6653 Faksi